ASUBUHI NA MAPEMA

Ngazi ya Kwanza

Tune salim

21st Century Basic Education Program(TZ21)
P O Box 34618
Dar es salaam

© Tune Salim,2014

Mchoraji: Abdul Gugu
Usanifu: Sisi Illustrators

ISBN 978 9987 9448 3 5

Kitabu hiki kimechapishwa na TZ21 kwa msaada wa watu wa marekani kupitia Shirika la Misaada la Marekani (USAID) na kuwezeshwa na Creative Associates International.Yaliyomo katika kitabu hiki yanatokana na mwandishi na mchapishaji wake na hayawakilishi maoni na msimamo wa USAID wala serikali ya Marekani.

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kuiga, kunakili, kutafsiri,Kupiga chapa au kukitoa kitabu hiki sehemu yake kwa njia yoyote ile bila idhini ya 21st Century Basic Education Program(TZ21)

Asubuhi na mapema naamka kitandani.

Asubuhi na mapema nasalimia wazazi.



Asubuhi na mapema napiga mswaki wangu.

Asubuhi na mapema naoga kwa maji safi.

Asubuhi na mapema napaka mwili mafuta.

Asubuhi na mapema naivaa sare safi.

Asubuhi na mapema natandika kitanda changu.

Asubuhi na mapema ninafungua kinywa.



Asubuhi na mapema nakimbilia skuli.

Zoezi:

1. Chagua jibu sahihi:
   (a) Wakati gani tunaamka?
      (i) Asubuhi
      (ii) Usiku
   (b) Baada ya kuamka tunafanya nini?
      (i) Tunapiga mswaki
      (ii) Tunafungua kinywa
   (c) Tunaoga kwa kutumia nini?
      (i) Maji
      (ii) Maziwa
2. Jibu maswali yafuatayo:
   (a) Tupake kitu gani ili mwili wetu uwe laini?
   (b) Nguo za aina moja tunazovaa skuli zinaitwa nini?

3. Taja mambo matatu unayo yafanya baada ya kuamka
   (i) _____
   (ii) _____
   (iii) _____

4. Ili chumba kiwe safi tufanyeje?

Msamiati:

piga mswaki: sugua meno kwa kutumia mswaki
paka: kueneza majimaji mfano mafuta ama losheni mwilini
sare: nguo za aina moja zivaliwazo skuli, kazini ama kwenye shughuli yoyote ile.
Kufungua kinywa: kula chakula cha kwanza baada ya kuamka

Fumbua fumbo hili kwa kumalizia herufi zinazokosekana

1. (a) Kwenda kulia: Kitu unachopaka mwilini ili uwe laini baada ya kuoga
   (b) Kwenda chini: kifaa unachutumia kusafisha meno
2. Shituka kutoka usingizini
3. (a) Kwenda kulia: Nguo za aina moja tunazovaa skuli
   (b) Kwenda chini: mahali tunapopata elimu
4. Yamo mdomoni mwetu na tunayatumia kwa kutafuna
5. Kwenda kulia: Tunatumia kwa kuogea, kunywa, kufulia, kuoshea vyombo
6. Kwenda chini: Kinyume cha mtu mzima
7. Kwenda kulia: Weka chumba katika hali ya usafi kufagia na kupiga deki
8. Kwenda chini: Muda tunaoamka.